**2 APRILI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 2 Aprili, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI ZILIIMBWA**

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Taarifa ya Spika na ninazo taarifa mbili; Taarifa ya kwanza inatolewa chini ya Kanuni ya 39(2) ya Kanuni zetu za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, mnamo tarehe 29 Februari, 2024 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, akilihutubia Taifa kupitia vyombo vya habari alitangaza kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu wa Zanzibar na Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mzee Ali Hassan Mwinyi, kilichotokea saa 11.30 jioni katika Hospitali ya Mzena, Jijini Dar es Salaam ambako alikuwa amelazwa kwa ajili ya matibabu ya saratani ya mapafu.

Waheshimiwa Wabunge, katika taarifa hiyo, Mheshimiwa Rais aliutaarifu umma kuwa Hayati Mzee Ali Hassan Mwinyi alikuwa akipatiwa matibabu tangu Novemba, 2023 Jijini London nchini Uingereza, baadaye alirejea nchini kuendelea na matibabu katika Hospitali ya Mzena hadi umauiti ulipomkuta. Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Rais alitoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na kwa Watanzania wote kwa ujumla kwa msiba huu mkubwa ambao Taifa letu lilikuwa limeupata. Aidha, alitangaza siku saba za maombolezo ambapo bendera zilipepea nusu mlingoti kuanzia tarehe 1 Machi, 2024.

Hayati Mzee Ali Hassan Mwinyi aliagwa rasmi katika Viwanja vya Uhuru tarehe 1 Machi, 2024 ambapo Watanzania walipata nafasi ya kutoa heshima zao za mwisho. Vilevile wananchi na viongozi wa Visiwani Zanzibar walipata nafasi ya kutoa heshima zao za mwisho tarehe 2 Machi, 2024 katika Uwanja wa Amani – Zanzibar na mazishi yalifanyika siku hiyo hiyo katika Kijiji cha Mangapwani huko Unguja, Zanzibar.

Waheshimiwa Wabunge, Hayati Mzee Ali Hassan Mwinyi ameitumikia nchi yetu katika nafasi mbalimbali ikiwemo kuwa Mbunge, Waziri na Rais wa Awamu ya Tatu wa Zanzibar kuanzia Januari, 1984 mpaka Oktoba, 1985. Aidha, alikuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1985 mpaka 1995. Hayati Mzee Ali Hassan Mwinyi atakumbukwa kwa kuonesha ujasiri na uwajibikaji pale alipojiuzuru kwa hiari katika nafasi ya Uwaziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mwaka 1976 kufuatia changamoto zilizojitokeza kwenye Wizara yake. Pia atakumbukwa kwa mageuzi makubwa aliyoyasimamia ya kuanzishwa kwa demokrasia ya vyama vingi na uchumi huria na kusababisha Watanzania kumtambua kwa jina la Mzee Rukhsa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu natoa pole kwa wake wa mzee wetu, Mama Siti Mwinyi na Mama Khadija Mwinyi, watoto wake wakiongozwa na Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi pamoja na Wabunge wenzetu Mheshimiwa Kepteni Abbas Ali Mwinyi na Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi,

ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa msiba huu mzito kwa Taifa letu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima ya mpendwa wetu naomba sasa tusimame kwa dakika moja kumkumbuka na kumuomba Mwenyezi Mungu ampokee na ampumzishe kwa amani.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walismama kwa dakika moja kumuombea Hayati Ali Hassani Mwinyi)*

**SPIKA:** Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ilikuwa ni taarifa ya kwanza, lakini ninayo taarifa nyingine ambayo inatolewa chini ya Kanuni ya 39(1) ya Kanuni zetu za Kudumu za Bunge. Katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada minne ya sheria ifuatayo: -

(a) Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023;

(b) Muswada wa Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023;

(c) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 *(The Political Parties Affairs Laws Amendment Bill, 2023);* na

(d) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2023 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment (No. 5) Bill 2023)*.

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa hii napenda kuriarifu Bunge hili Tukufu kuwa tayari Miswada hiyo minne imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuwa sheria za nchi. Sasa hizi zimekuwa sheria za nchi na zinaitwa majina yafuatayo:-

(a) Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani (Na. 1) ya Mwaka 2024;

(b) Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (Na. 2) ya Mwaka 2024;

(c) Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa (Na. 3) ya Mwaka 2024 *(The Political Parties Affairs Laws Amendment Act No. 03 of 2024);* na

(d) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) ya Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment Act (No. 4) of 2024)*.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo hizi zimekwishakuwa sheria kamili, Mheshimiwa Rais ameshafanya kwa sehemu yake.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya taarifa hiyo tunaendelea na ratiba iliyopo.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

(i) Fungu 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu;
(ii) Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu;
(iii) Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa;
(iv) Fungu 42 - Ofisi ya Bunge;
(v) Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi;

(vi) Fungu 65 - Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu;
(vii) Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA);*
(viii) Fungu 91 - Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya; na
(ix) Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali na tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 1

### Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Shitage - Uyui

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Shitage – Uyui kilichoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na kituo cha afya katika Kata ya Shitage. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Uyui imetenga shilingi milioni 350 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya vya Mabama, Loya, Tuura pamoja na Zahanati za Ibela, Mbiti, Izugawima, Gilimba na Magir.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Uyui itatenga bajeti kwa ajili ya ukamilishaji wa Kituo cha Afya cha Shitage, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwa kuwa kituo hiki cha Shitage kinachojengwa kwa kutumia nguvu za wananchi kimechukua muda mrefu, vilevile, kwa kuwa kituo kipo mbali kwa umbali wa kilometa 120 mpaka kituo kingine cha afya na kitahudumia kata tatu ambazo ni Shitage, Igulungu na Bukumbi; je, Serikali haioni kwamba umefika muda sasa wa kujenga kituo hiki ili kitoe huduma kwa hizi kata tatu?

Swali la pili, kwa vile kituo hiki cha Shitage Mheshimiwa Waziri anasema inategemea fedha za ndani za mwaka 2025/2026 zianze kujenga kituo hiki, wananchi wamechoka; haoni kwamba ni mbali sana kufikiria kujengewa tena kwa fedha za ndani za Halmashauri mpaka mwaka 2025/2026 ni mbali sana. Je, haoni umuhimu wa kumaliza kituo hiki sasa hivi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua kuwa kituo hiki cha Shitage kiko mbali na kinahudumia takribani kata tatu na ndiyo maana imeweka kipaumbele cha kutenga fedha katika bajeti ijayo ya mwaka 2025/2026 kwa ajili ya kukamilisha kwa sababu katika mwaka huu

wa fedha na mwaka ujao wa fedha tunakwenda kukamilisha vituo viwili vya afya na zahanati nne.

Mheshimiwa Spika, pili, mwaka 2025/2026 siyo mbali kwa sababu safari ni hatua na tumekwishaanza ujenzi wa vituo vingine hivyo tutakamilisha ujenzi wa kituo hicho muda huo ukifika, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaona mmesimama na mnafahamu kuwa kipindi hiki cha Bunge la Bajeti maswali huwa ni saa moja. Maswali mafupi, ukiendelea hapa mbele nabonyeza kama Waziri hajasikia tunasonga kwa mwingine. Ukishaanza na habari za kwa kuwa, kwa sababu, kwa kuwa, kulikuwa tayari kuna changamoto hapo, nenda moja kwa moja kwenye swali ili na wenzako wapate nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ni lini Kituo kipya cha Iramba Ndogo kitakamilika na kutumika kama kilivyokusudiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali itatenga fedha kwa kupitia mapato ya ndani, lakini pia Serikali Kuu kwa ajili ya kukamilisha kituo hicho cha afya katika mwaka ujao wa fedha wa 2025/2026 kwa sababu tayari maombi yameshawasilishwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Zahanati Maalum ya Fulwe itakamilishwa jengo la mama na mtoto ambalo limejengwa kwa nguvu za wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeweka utaratibu wa kutambua vituo vya afya, zahanati na kujenga kwa awamu. Kwa hiyo, naomba nichukue ombi la Mheshimiwa Mbunge, tukafuatilie hatua za utekelezaji wa zahanati hiyo na baada ya hapo tutatafuta fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati.

**SPIKA:** Haya na mimi salamu za shukrani nimeshazipokea, kwa hiyo, tunakomboa wakati. Usinishukuru, nimeshakupa nafasi, nimeshazipokea tayari.

Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kabwe Wilaya ya Nkasi Kaskazini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Kabwe katika Halmashauri ya Nkasi ni moja ya vituo ambavyo vipo kwenye mpango mkakati wa kujenga na kukamilishwa kwa awamu. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi kuanza kutenga fedha ya mapato ya ndani, lakini pia kuleta hoja hiyo Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kupata fedha, ahsante.

**SPIKA;** Mheshimiwa Tabasam, swali la nyongeza.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kufuatana na mimi kwenda Sengerema kwenda kuangalia maboma ya zahanati ambazo hazijakamilishwa kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, niko tayari na baada ya maswali na majibu nitakufuata hapo ili tuweze kupanga ratiba ya kwenda huko.

**SPIKA:** Sasa naona mnasimama hadi ambao hamkuwa mmesimama mwanzoni kabisa. Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya katika Kata ya Uyui, Manispaa ya Tabora Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nimuombe Mheshimiwa Mbunge, lakini nimwelekeze Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora kuwasilisha, kwanza vigezo vya kata hiyo kama inahitaji kituo cha afya cha kimkakati, lakini pia kutupa mpango wa ndani wa halmashauri kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi wakati Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ukamilishaji, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatuletea vifaa tiba na dawa katika zahanati mbili ambazo zimekamilika katika Kijiji cha Mwangaza na Kijiji cha Namali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatoa fedha zaidi ya shilingi bilioni 190 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya, lakini pia uwekaji wa vifaa tiba katika zahanati zetu zikiwemo zahanati za Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo. Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba

tutafuatilia tuone katika ile shilingi milioni 600 iliyokwenda Namtumbo fedha ambayo inatakiwa kwenda kuweka vifaa tiba katika zahanati hizo mbili kama imepelekwa ili vifaa vipelekwe mapema wananchi waanze kupata huduma, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya ya Nyambiti ambapo ujenzi wake ulianza kwa nguvu za wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Serikali ilishaweka mkakati wa uhakika kabisa kuhakikisha majengo yote ya vituo vya afya yale muhimu yakiwemo majengo ya upasuaji yanakamilishwa na kuanza kutoa huduma. Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI, lakini pia na halmashauri tutahakikisha pale Sumve kile kituo cha afya kinakamilika ili jengo la upasuaji lianze kutoa huduma kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, Serikali ilitupa karatasi tukajaza vituo vya kimkakati, je, ni lini vituo vya Halmashauri ya Itigi vitaletewa fedha ili tujenge kituo cha kimkakati cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Waheshimiwa Wabunge waliorodhesha maeneo ya kujenga vituo vya afya vya kimkakati ikiwemo katika Halmashauri ya Manyoni pale Itigi. Nimhakikishie Mheshimiwa

Mbunge kwamba Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kujenga vituo hivyo vya afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, nataka kujua ni lini Serikali itajenga…

**SPIKA:** Weka kisemeo chako vizuri.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya katika Kata ya Ijangalo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ili kujenga kituo cha afya kuna vigezo ambavyo ni muhimu viwe vimezingatiwa. Kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutawasiliana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chemba ili tuweze kuona kata hiyo kama inakidhi vigezo ili tuanze kutafuta fedha za mapato ya ndani na Serikali Kuu kwa ajili ya kujenga kituo hicho cha afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Wananchi wa Mbogwe walijenga maboma kila kijiji na mpango wa Serikali ni kwamba Serikali itakuja kuwashika mkono ili kusudi kuyamalizia maboma yale.

Je, ni lini sasa Serikali itatoa pesa ili kusudi maboma yaliyojengwa na wananchi yaweze kukamilika ili waweze kupata tiba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kipindi cha miaka mitatu imetoa zaidi ya shilingi bilioni 450 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati zikiwemo zahanati hizi za Jimbo la Mbogwe. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba safari ni hatua, tunaendelea kwa awamu wameshapata nadhani tutatendelea kukamilisha maboma yaliyobakia, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, yameulizwa maswali mengi sana kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nini mkakati wa Serikali kujenga kituo cha afya kwenye Kata ya Mtunda pale Kibiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kujenga vituo vya afya kwenye maeneo ya kimkakati ambayo yamekidhi vigezo, kwa hiyo, naomba tuichukue hili ambalo Mheshimiwa Mpembenwe amelisema tukafanye tathmini ya kata hiyo kama inakidhi vigezo ili Serikali itafute kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo vya afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza. Limeshaulizwa? Haya basi. Haya ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, maswali mengine yapo huku mbele hili ni swali la kwanza tu, ahsante sana.

Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 2

**Zahanati ya Solwa kuwa Kituo cha Afya**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ahadi yake ya kuifanya Zahanati ya Solwa iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kuwa kituo cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Zahanati ya Solwa ilianza kutoa huduma mwaka 1964. Aidha, eneo ilipojengwa zahanati lina ukubwa wa ekari 1.5 ambalo halitoshelezi kwa ujenzi wa miundombinu ya kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeelekeza uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kutafuta eneo lenye ukubwa wa kuanzia ekari 15 ambalo litawezesha ujenzi wa kituo cha afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi na ikawaambia wananchi watumie nguvu zao kuhakikisha wanajenga kituo cha afya, wamejenga wameweka wodi mbili pamoja na *OPD*.

Je, kwa kuwaambia hivyo Serikali haioni kwamba inawasumbua wananchi na kuwakatisha tamaa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa wamekwisha kujenga sehemu ambayo ni ndogo na Kata ya Solwa ina wakazi 32000; je, Serikali itawafidia kujenga sehemu nyingine kwa gharama zote za Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Solwa kwamba Serikali inathamini sana kazi kubwa waliyofanya kwa nguvu zao kwa ujenzi wa Jengo la *OPD* na wodi.

Mheshimiwa Spika, kwa *standard* za Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa sasa zahanati pia zinakuwa zina wodi, lakini sababu kubwa eneo ni dogo, ekari 1.5 ni ndogo sana kujenga kituo cha afya kwa sababu tunatazama miaka 50, 100 ijayo. Kwa hiyo, niwahakikishie kwamba zahanati hiyo ambayo wamejenga itasajiliwa, itaanza kutoa huduma kama zahanati na kuendelea kutoa huduma hizo, lakini Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kujenga kituo cha afya katika eneo ambalo Mkurugenzi ameelekezwa kulitafuta kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatupatia fedha kujenga *mortuary* na wodi ya kujifungulia wanawake katika Kituo cha Afya Ndalambo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Ndarambo ni kweli kina upungufu wa wodi na jengo la kuhifadhia maiti. Serikali ilikwisha mwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Momba kuanza kutenga fedha kwa awamu kupitia mapato ya ndani, lakini na Ofisi ya Rais, TAMISEMI inatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kuunga mkono ukamilishaji wa majengo hayo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge

kwamba Serikali inatafuta fedha na tutakwenda kujenga majengo hayo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali italeta pesa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ukamilishaji wa Vituo vya Ndabusozi na Kalenge kama ilivyoahidiwa katika bajeti ya mwaka huu tunaoendelea nao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, vipo vituo vya afya ambavyo vilipokea shilingi milioni 250 na ujenzi wake haujakamilika kwa sababu tunahitaji shilingi milioni 250 nyingine. Kwa hiyo, vituo vyote, vikiwemo hivyo vya ndani ya Jimbo la Biharamulo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Chiwelesa kwamba Serikali ina mpango mkakati wa kupeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha vituo hivyo vya afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itakamilisha Zahanati ya Kijiji cha Ilulu kilichopo Kata ya Isongole Wilayani Ileje, ili wananchi waweze kupata huduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali ilishaelekeza Wakurugenzi kuweka kipaumbele cha ukamilishaji wa miundombinu ya huduma za jamii vikiwemo vituo vya afya na zahanati kama kipaumbele kwenye bajeti zao. Katika bajeti ya mwaka huu 2024/2025 wameelekezwa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma. Kwa hiyo, naomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge, tutafuatilia kupitia mapato ya ndani ya halmashauri. Pia katika zile fedha za maboma matatu

kila jimbo na kila Halmashauri tutahakikisha fedha hiyo inakwenda pale kwa ajili ya ukamilishaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapeleka huduma za *theatre, x-ray* na vitanda vya kuzalisha katika Kituo cha Afya cha *Mkwawa University*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeshapeleka fedha nyingi katika halmashauri zetu. Waheshimiwa Wabunge ni mashuhuda katika mwaka huu wa fedha karibu kila halmashauri imepata si chini ya shilingi milioni 600 kwa ajili ya kununua vifaa tiba vya majengo ya upasuaji lakini pia *x-ray* zimepelekwa za zaidi ya shilingi bilioni 93. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hili ni endelevu na tutahakikisha kituo cha afya hicho pia kinapata vifaa tiba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abbas Tarimba, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Tandale kinahudumia watu kati ya 800 hadi 1000 kwa siku.

Serikali ina mpango gani katika kukipanua kituo hiki na kukiongezea uwezo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa bahati nzuri nilipokuwa Mganga Mkuu wa Manispaa ya Kinondoni tulikubaliana kwamba tununue lile eneo lililoko nyuma ya Kituo cha Afya cha Tandale, kwa hiyo, ninaamini lile eneo bado lipo. Tulishamwelekeza Mkurugenzi kuhakikisha wanatenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa fidia ya eneo lile ili kuongeza eneo la ujenzi wa Kituo cha Afya cha

Tandale. Kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii kimuelekeza na kumsisitiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni kufanya hivyo, kwa sababu ni muhimu sana kwa wananchi wa Tandale, na kituo kile kiko katika eneo ambalo ni *potential* sana kutoa huduma za afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Tarafa ya Nampungu kilipokea shilingi milioni 250 na majengo haya yamekamilika na yako *idle* kwa muda mrefu.

Je, ni lini Serikali itatuongezea shilingi milioni 250 ili kukamilisha kituo kile?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vituo vyote vya afya vilivyopokea fedha shilingi milioni 250 vimeandaliwa katika bajeti kupelekewa fedha nyingine shilingi milioni 250 kwa awamu ili majengo yote yakamilike, kikiwemo kituo cha afya ambacho kipo katika Jimbo la Tunduru Kusini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Zahanati ya Kihwera iliyopo katika Kata ya Kabilizi itapandishwa hadhi na kuwa kituo cha afya, kwa sababu inahudumia watu wengi zaidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ili zahanati ipandishwe hadhi kuwa kituo cha afya kuna vigezo ambavyo vinazingatiwa, ikiwemo idadi ya wananchi wanaohudumiwa, ukubwa wa eneo, lakini pia uwepo wa

miundombinu inayotosheleza kituo cha afya. Kwa hiyo, ninaomba nilichukue jambo hili ili Ofisi ya Rais, TAMISEMI iweze kufuatilia. Lakini nimwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muleba kuleta taarifa rasmi kama eneo lile linakidhi vigezo na zahanati ile inakidhi vigezo vya kupandishwa kuwa kituo cha afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati kwenye maeneo ya Mashoa na Vugiri kwa sababu haya yamekidhi vigezo na tumeyaainisha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba kila mwaka wa fedha kila bajeti inapotengwa tunatenga vituo vya afya vya kimkakati na vinaendelea kujengwa kwa awamu nchini kote. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba katika Jimbo la Korogwe Vijijini pia tunatenga fedha hizo kwa ajili ya kujengo vituo hivyo vya afya vya kimkakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH LEMBURIS S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itatoa fedha za kupanua Zahanati ya Kiyoga katika Kata ya Ikidimwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, majengo ya zahanati yana *standard* zake na ikiwa zahanati ina miundombinu pungufu ya ile inayotakiwa kwa mujibu wa vigezo vyetu tuna utaratibu wa kutenga fedha kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya upanuzi. Lakini kama halmashauri haina uwezo basi

inaomba Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya utekelezaji huo. Kwa hiyo, naomba nimwelekeze pia Mkurugenzi wa Arumeru waanze kutenga fedha kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya upanuzi wa zahanati hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale, swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya cha Ngerengere maana hatuna jengo la mama na mtoto wala sehemu ya kuhifadhia maiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Kituo cha Afya cha Ngerengere hakina jengo la mama na mtoto, lakini pia hakina jengo la kuhifadhia maiti. Tulishawasiliana na Mheshimiwa Taletale na tumekubaliana kuanza kutenga fedha kwa awamu kupitia mapato ya ndani, lakini pia kupitia Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi huo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha na itaenda kujenga majengo hayo kwa awamu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ni lini Vituo vya Afya vya Kasiguti na Kisole vitakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, vituo hivyo vya afya ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja sina taarifa kwa nini havijakamilika. Aidha, fedha hazijafika au hazijatumiwa vizuri. Kwa hiyo, naomba nilifuatilie niweze kujua hali halisi ikoje ili Ofisi ya Rais, TAMISEMI iweze kujua hali halisi ikoje ili Ofisi ya Rais, TAMISEMI tuweze kutoa maelekezo kuhakikisha

kwamba vituo hivyo vinakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, swali la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itaifanya Zahanati ya Hedi kwa Magome kuwa kituo cha afya kama Waziri wa TAMISEMI alivyoahidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kadri ya ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuongeza miundombinu kutoka zahanati ili iweze kukidhi ngazi ya kuwa kituo cha afya. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kulifanyia kazi jambo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 3

**Serikali kutangaza maeneo mapya ya kiutawala**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatangaza maeneo mapya ya kiutawala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa maeneo mapya ya utawala huzingatia Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya, Sura 287 na Sheria ya Mamlaka za Miji, Sura 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imetoa kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha miundombinu kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadaye kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza, kwa kuwa Serikali ilipeleka mwongozo kwenye kata zetu na kwenye majimbo na viongozi kwenye maeneo mbalimbali wakajadili na kupendekeza maeneo mapya ya kiutawala na kama haya ndiyo majibu ya Serikali.

Je, Serikali ipo tayari kupeleka mwongozo wa kufuta ule ambao walipeleka kwamba tutapendekeza maeneo ili kupunguza usumbufu na maswali kwa Waheshimiwa Wabunge?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna ahadi kwenye jimbo langu pale mamlaka ya mji maeneo mawili, Sirari na Nyamongo, kwa msimamo wa Serikali huo.

Je, ni nini kauli ambayo sasa watu wa Tarime wataambiwa juu ya ahadi za viongozi wakuu ambazo zilitolewa tangu mwaka 2011 mpaka leo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, swali la pili anaweza akarejea sijalisikia vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni hivi kule katika Jimbo la Tarime Vijijini eneo la Sirari na Nyamongo Waheshimiwa Mawaziri Wakuu kuanzia Mzee Pinda na Waziri Mkuu wa sasa, Mheshimiwa Kassim Majaliwa waliahidi kutoa Mamlaka ya Mji katika maeneo hayo.

Kwa majibu ya Serikali, lini sasa watu wa Sirari na Nyamongo wategemee kupata mamlaka za miji katika maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli Serikali ilipeleka mwongozo wa namna ambavyo vikao vya kisheria vinatakiwa kukaa kwa ajili ya kuanzisha mamlaka mpya katika maeneo yetu. Mwongozo huo ni halali mpaka sasa kwa sababu Serikali haijafuta dhamira ya kuongeza maeneo hayo. Michakato inaendelea kama kawaida, inawasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na muda utakapofika kwa ajili ya kutenga maeneo mapya kazi itakayofanyika na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni kupitia maombi ambayo tayari yamekwisha kuwasilishwa na mamlaka mbalimbali kote nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hatuna sababu ya kufuta mwongozo kwa sababu zoezi ni endelevu, linaendelea lakini muda ukifika tutakuwa tuna kazi tu ya kupitia yale maombi yamekwisha kuletwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pili kuhusiana na uanzishwaji wa mamlaka ya mji ni utaratibu ule ule kwamba baada ya kukamilisha miundombinu katika mamlaka zilizopo tutakwenda sasa kuanzisha mamlaka nyingine na wakati huo tutalifanyia kazi suala hilo ambalo ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, mimi nauliza, eneo la jimbo siyo eneo la utawala bali ni eneo la uwakilishi na kuna majimbo ambayo ni makubwa mno kama Jimbo la Sikonge na tayari tumeshawasilisha kwenye vikao vyote vya wilaya na mkoa, tumeipitisha.

Je, Serikali ina mtazamo upi katika kuhakikisha kwamba majimbo yanagawiwa ili kuanzisha majimbo mapya kwenye majimbo makubwa zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tukizungumzia majimbo makubwa sana pia kuna majimbo madogo sana, lakini pia hii hoja ya mgawanyo wa majimbo siyo ya TAMISEMI. Siyo hoja ya TAMISEMI, hoja ya mgawanyo wa majimbo kama Serikali inayo majibu itoe kama haina siyo swali la TAMISEMI.

Kwa hiyo, lije liulizwe kama swali la msingi ili tupate majibu ambayo yatatupeleka sehemu nzuri. Alikuwa amesimama pia Mheshimiwa Justin Nyamoga. *(Makofi)*

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ilula ina zaidi ya miaka 20 sasa; je ni mpango Serikali inao wa kuhakikisha kwamba inakuwa halmashauri kamili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kweli Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ilula ina umri mrefu haijapanda kuwa Halmashauri ya Mji, lakini zipo mamlaka nyingi ndogo katika nchi yetu ambazo pia zina umri mrefu. Zipo mamlaka ambazo hazikidhi vigezo vya kuwa halmashauri, Serikali inaendelea kufanya uchambuzi, lakini zipo ambazo zinakidhi kuwa Halmashauri za Miji. Kwa hiyo, naomba nilichukue suala hili ili muda ukifika tutakuwa tumeshafanya tathmini kama Mamlaka ya Ilula inakidhi haja ya kuwa halmashauri basi itapata sifa hizo baada ya Serikali kuamua kuanza kupandisha hadhi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, sasa aulize swali lake.

Na. 4

**Serikali kupeleka walimu wa kutosha kwa shule mpya - Vwawa**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka walimu wa kutosha katika shule mpya kumi za msingi na sekondari zilizojengwa Vwawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari, 2024 Serikali imepeleka jumla ya walimu 33 wa shule za msingi na walimu 32 wa shule za sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kwa ajili ya shule mpya. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuajiri na kuwapangia vituo walimu mara baada ya taratibu za kibali kutoka Ofisi ya Rais, Utumishi kukamilika ili kuboresha ikama katika shule za msingi na sekondari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi, hesabu na biashara ambayo ni 172 katika shule za sekondari mpya; na kwa kuwa katika shule za msingi kuna upungufu wa walimu 693.

Je, zipi hatua za Serikali za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu wa kukabiliana na changamoto hii ya upungufu wa walimu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa katika maeneo mengi kuna walimu wengi ambao wamehitimu na bado hawana ajira, upi mkakati wa Serikali wa kuwatumia hao walimu kwa muda mfupi ili waweze kusaidia katika kupunguza changamoto ya upungufu wa walimu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kweli katika shule zetu kote nchini zikiwemo shule hizi za Jimbo la Vwawa kuna upungufu wa walimu wa sayansi, hisabati lakini na masomo mengine kama masomo ya biashara, lakini Waheshimiwa Wabunge ni mashuhuda kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeajiri walimu kwa wingi kwa makumi elfu katika kipindi cha miaka hii mitatu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo walimu wameendelea kuajiriwa na kupelekwa katika shule hizo Serikali itaendelea kuajiri kadri kibali cha ajira kinavyojitokeza na kipaumbele cha ajira hizi huwa ni walimu wa sayansi, walimu wa hisabati na masomo mengine yenye upungufu mkubwa zaidi. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge zoezi hilo linaendelea na tutahakikisha kwamba walimu wanafika kupunguza upungufu wa walimu katika shule hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, Serikali ilishatoa mwongozo wa namna ambavyo halmashauri zinaweza kutumia mapato ya ndani kuingia mikataba na walimu ambao wamehitimu wako katika maeneo yao kwa ajili ya kufundisha. Sisi sote tumeshuhudia kote nchini shule nyingi zina walimu ambao wameajiriwa kwa mikataba na wanaendelea kufundisha wakisubiri ajira za kudumu.

Nitumie nafasi hii kusisitiza na kuhamasisha Wakurugenzi wahakikishe wanatumia fursa hii vizuri, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mmesimama wengi, lakini tukubaliane kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri ameulizwa maswali mengi sana, kwa hivyo sitawaruhusu wengi kama ambavyo mmesimama, nitawaruhusu Wabunge wachache tu.

Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru; Halmashauri ya Mji Njombe ambayo ina vijiji na miji, mwaka jana haikupata mgao kama halmashauri nyingine za miji ambazo zina vijiji; je, Serikali ina mpango gani kwenye mgao wa safari kuzifikiria tofauti ili zipate walimu wa kutosha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, wakati wa kupeleka walimu katika vituo vyetu baada ya ajira kuna vigezo ambavyo vinazingatiwa lakini kigezo muhimu ni upungufu mkubwa zaidi wa walimu katika halmashauri hizo na katika shule hizo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mara ajira zitakapojitokeza tutahakikisha tunazingatia vigezo na yale maeneo ambayo yana upungufu mkubwa katika halmashauri ya Mji wa Njombe yatapelekewa walimu ili kupunguza *gap* hiyo ya walimu katika shule hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna upungufu mkubwa sana wa nyumba za walimu; je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga maboma yote ya nyumba za walimu katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu na kwingineko nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba kuna upungufu mkubwa wa nyumba za walimu na tayari imeshaanza mkakati na utekelezaji unaendelea wa kujenga nyumba za *three in one, two in one* katika shule zetu lakini pia maboma ya nyumba za walimu katika shule zetu yameshaanza kutambuliwa yote na kuna mpango kabambe wa kuhakikisha shule zinakuwa na nyumba za walimu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hilo litafanyika na walimu wetu watapata nyumba katika shule hizo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bukoba Mjini inahitaji walimu wa sayansi 386 lakini hivi sasa kuna walimu 146, hivyo tuna upungufu wa walimu wa sayansi 240.

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba Bukoba Mjini tunapata walimu wa sayansi wa kutosha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bukoba Mjini ni moja ya halmashauri ambazo katika ajira zote za walimu zilizopita pia walipata walimu wa masomo ya sayansi, lakini ni kweli kwamba walimu wale bado hawatoshelezi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kila ajira zitakapojitokeza tutahakikisha tunaipa kipaumbele Halmashauri ya Bukoba Mjini ili walimu wa sayansi waweze kupatikana na kuboresha ikama katika shule zetu zote, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 5

**Marekebisho ya Sheria ya Mazingira**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawasilisha Marekebisho ya Sheria ya Mazingira ili kuipa *NEMC* uwezo wa hadhi ya mamlaka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza, majibu.

Samahani, nimekutaja kwa cheo chako cha zamani, nisije nikakurejesha huko.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Mwinyi Azan, Mbunge Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kusini Pemba, najibu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Ofisi ya Makamu wa Rais ipo katika mchakato wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191. Katika marekebisho hayo, kubadili muundo wa Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* na kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira *(NEMA)* ni moja ya masuala yanayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ili *NEMC* iweze kuwa Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwamba hadi kufikia Juni 2024, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 uwasilishwe katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa unayekatiza kati ya anayezungumza na mimi, rudi kwenye siti uliyokuwa umekaa kabla. Rudi huku mbele ulikokuwa umekaa kabla. Enhee, keti, haya, umeshaketi.

Mheshimiwa endelea na swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, je baada ya mabadiliko ya sheria, majukumu ya mameneja wa kanda wa *NEMC* yatabadilika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika marekebisho hayo je, mna mkakati gani wa Serikali *ZEMA* na *NEMC* kufanyakazi kwa pamoja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maryam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa mujibu wa sheria hii ya *NEMC* tumeteua mameneja wa kanda ambao wanasimamia kwenye kanda zao zikiwemo Kanda za Ziwa, Kanda za Kusini na Kanda ya Dar es Salaam na kanda nyingine.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii hapa mbele ya Bunge lako Tukufu niwapongeze sana mameneja wetu wa kanda zote za *NEMC* kwa kufanya majukumu yao na kusimamia vizuri.

Majukumu haya yanaweza yakaongezeka lakini pia yanaweza yasibadilike kikubwa itategemea sheria hii itakavyopendekeza. Hatujajua Wabunge na wadau wengine watakuja na mapendekezo gani lakini kikubwa majukumu yao ni kusimamia sheria, majukumu yao ni kutoa elimu kwa jamii na kufanya majukumu mengine yatakavyoelekezwa kama sheria itakavyotaka. Kwa hiyo, nadhani sheria itakapokuja ndivyo itakavyoonyesha mabadiliko ama kuongezeka kwa majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili niseme tu kwamba *ZEMA* na *NEMC* wamekuwa ama tumekuwa tukifanya kazi ya ushirikiano wa karibu kwa muda mrefu lakini hata mabadiliko haya ya sheria yatakapokuja moja ya miongoni mwa msisitizo wake katika sheria hii yatasisitiza *ZEMA* na *NEMC,* ama *ZEMA* na *NEMA* kufanyakazi kwa pamoja zikiwemo kazi za utoaji wa elimu na kazi za usimamiaji wa sheria na kazi nyingine za masuala ya usimamizi na uhifadhi wa mazingira, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 6

**Hasara kwa wakulima msimu 2022/2023**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, Serikali imefanya utafiti kubaini sababu zilizopelekea wakulima kupata hasara katika mavuno ya mwaka 2022/2023?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imekuwa ikiratibu na kufanya tathmini ya uzalishaji na upatikanaji wa chakula nchini. Lengo la tathmini ni kuiwezesha Serikali kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha utengamano wa hali ya usalama wa chakula nchini unaimarika.

Mheshimiwa Spika, kupitia tathmini hiyo, uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa msimu wa mwaka 2022/2023 ulikuwa tani 20,402,014 ambapo mahitaji ya chakula ni tani 16,390,404 sawa na utoshelevu wa asilimia 124. Pamoja na mafanikio hayo, changamoto mbalimbali zilijitokeza na kusababisha hasara kwa baadhi ya wakulima nchini. Miongoni mwa changamoto hizo ni mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha unyeshaji mvua kwa mtawanyiko usioridhisha, matumizi madogo ya teknolojia na milipuko ya visumbufu vya mazao shambani hususan viwavi jeshi na kwelea kwelea kwenye baadhi ya mashamba ya wakulima nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali yanaonesha hakuna tafiti zinazofanyika kila msimu wa kilimo na ndiyo maana majibu yanaonesha hayajitoshelezi kulingana na changamoto ambazo tuliziona ambazo zilikuwa kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, hivyo nilitamani kufahamu…

**SPIKA:** Ngoja, nieleweshe vizuri, ukisema hayajitoshelezi, haya majibu yaliyotolewa wewe unaona ni majibu ya Serikali ama swali lako halijajibiwa ili ndio nijue kama nikuruhusu ya swali la nyongeza ama Serikali ije ijibu upya swali lako.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, majibu yangu yanaonesha kwamba hawajafanya tafiti kwa huo mwaka

nilioutaja. Kwa hiyo, inaonesha hawafanyi tafiti kubaini changamoto wanazokutana nazo wakulima kwa kila mwaka na tunapoongelea wakulima hatumaanishi mazao tu ya chakula, kuna mazao mengi nchi hii ambayo yanatakiwa yaendelee kuzalishwa vizuri.

**SPIKA:** Sasa wewe umeuliza swali mwaka 2022/2023, Serikali inasema kupitia tathmini hiyo uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa msimu wa mwaka 2022/2023 wewe takwimu ulizonazo ni tofauti na hizi za Serikali.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, iko hivi, msimu huu kulikuwa na changamoto nyingi ikiwemo mbegu *fake* kwa Mkoa wetu wa Songwe na ninachoongelea nilikuwa nimeuliza wamefanya tafiti? Sikuuliza kama wamefanya tathmini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo…

**SPIKA:** Haya, sasa basi uketi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Mbunge anasema yeye alikuwa anataka majibu ya utafiti, ninyi mmefanya tathmini na hapa mbele mimi sina kamusi ya kuonesha tofauti ya haya maneno ya tathmini na utafiti lakini Mbunge anasema yeye ameuliza kuhusu utafiti.

Kwa hivyo, ili yeye moyo wake uridhike, haya maneno yalitokea hapa tathmini hili jibu mkalilete upya ili Mbunge ajue tathmini mmefanya na utafiti unaendana hivyo. Kwa sababu sasa hawezi kuuliza maswali ya nyongeza kwenye jibu ambalo yeye anasema aliomba utafiti nyie mmefanya tathmini. Kwa hiyo, hili tutaenda nalo kwa sura hiyo, sijui kama kuna swali lingine. Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani huna swali lingine.

Mheshimiwa Neema swali lako kwa sababu liliuliza utafiti na limejibiwa tathmini utajibiwa upya swali lako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, Mbunge wa Viti

Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Maimuna Pathan.

Na. 7

**Upandaji wa miti – Morogoro**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN K.n.y. MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupanda miti katika Mkoa wa Morogoro hususani Milima ya Uluguru na kandokando ya Mto Fulua, Mnyera na Kilombero?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aleksia Kamguna, kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha uhifadhi unaendelezwa katika Milima ya Uluguru, zoezi la kupanda miti limeendelea kufanyika katika Mkoa wa Morogoro hususani katika milima hiyo. Mathalani, kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)* kwa kushirikiana na halmashauri na wadau mbalimbali imepanda jumla ya miti 9,026,605 ikiwemo miti 1,000,000 ya mikarafuu kwa ajili ya viungo katika mpaka wa msitu wa Mazingira Asili Uluguru, pamoja na vijiji vinavyopakana na msitu huo na katika Mkoa wa Morogoro kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maeneo ya Mto Fulua, Mnyera na Kilombero, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, wananchi na wadau imeendelea na jitihada za kutunza maeneo hayo kwa kupanda miti rafiki wa maji

pamoja na kuendelea kutoa elimu ya umuhimu wa uhifadhi na kupanda miti stahiki katika maeneo ya kingo za mito.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani thabiti wa kukomesha ukataji miti hovyo? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali inawachukulia hatua gani wale waliobainika kukata miti hovyo na kusababisha nchi yetu kuwa jangwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TFS* imekuwa ikifanya doria mbalimbali za kuhakikisha ukataji miti hovyo unazuiliwa. Vilevile, imekuwa ikichukua hatua kwa wale wote ambao wamekuwa wakifanya vitendo hivi kuwafikisha Mahakamani kwa mujibu wa sheria ili kuchukuliwa hatua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga Mbunge wa Iramba Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 8

**Ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mkalama**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mkalama utaanza?

**SPIKA:** Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Mkalama, kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania imeendelea kuimarisha majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kujenga majengo mapya na kukarabati majengo chakavu. Wilaya ya Mkalama ni moja ya Wilaya nne ambazo kwa sasa bado huduma za Mahakama zinapatikana kupitia wilaya za jirani. Aidha, kutokana na uhaba wa majengo ya Mahakama, majengo haya yanajengwa na kukarabatiwa kwa awamu kwa kuzingatia uwezo wa kibajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mpango wa ujenzi na ukarabati wa Mahakama wa mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026 ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mkalama unatarajiwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka 2023/2024. Kwa sasa tayari maandalizi ya michoro hiyo yamekamilika na zabuni imetangazwa ili kupata mkandarasi wa ujenzi. Hivyo, ujenzi huo kimsingi unatarajiwa kuanza kabla ya mwezi Juni, 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali yanayotia moyo, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Wananchi wa Mkalama wamepoteza sana haki zao kwa kuamua kuachana na kesi kwa kukosa uwezo wa kwenda wilaya ya jirani kupata haki yao; na kwa kuwa bajeti yetu ni *cash budget;* je, Serikali inatoa *commitment* gani kuhakikisha kwamba mgao wa kwanza tu wa bajeti hii unakwenda Mkalama kuondoa tatizo hili ambalo limewasumbua sana wananchi wa Mkalama? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi Serikali iko makini na ujenzi wa Mahakama hii ya Mkalama. Hivi sasa kupitia Mkurugenzi tumeshalipa fidia, eneo lile kulikuwa na makaburi ikabidi kulipa fidia na kumwelekeza Mkurugenzi ahamishe makaburi. Kwa hiyo, tayari masuala ya *compensation* (fidia) yamekamilika na Serikali inatambua kabisa umuhimu wa huduma za mahakama kwa wananchi wetu (utawala wa sheria).

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba tangu Wilaya Mpya ya Mkalama imeanza, huduma zilikuwa bado zinatolewa kwenye Wilaya jirani ya Iramba tangu mwaka 2012. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari michoro imekamilika na kabla ya Juni, katika bajeti hii ambayo tunayo, tunatarajia kuanza hii kazi. Kama ulivyosema, mara pesa itakapopatikana, basi tuweke kipaumbele. Hilo tutalihakikisha tunalizingatia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, katika mwaka wa fedha 2023/2024 inaonesha kwamba Wilaya ya Kishapu itajengewa Mahakama ya Wilaya; ni lini ujenzi huo utaanza katika Wilaya ya Kishapu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kimsingi Mahakama ya Wilaya ya Kishapu ni miongoni mwa zile Mahakama ambazo ziko katika mpango mkakati wa kujengwa mwaka 2024/2025. Tunaishukuru sana Kamati ya Katiba na Sheria imepitisha pesa na hatua ya Mahakama ya Kishapu na yenyewe ipo katika maandalizi ya mchoro na Maandalizi hayo yameshakamilika na mzabuni ameshatangazwa ili kupata mkandarasi wa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, tuna imani kadiri fedha zinavyopatikana, kabla ya kwisha bajeti hii ya sasa ambayo inaisha Juni, 2024 Mahakama hii ya Kishapu pia itakuwa imeanza kujengwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2023/2024 Serikali ilionesha kwamba inaenda kujenga Mahakama yenye hadhi ya kiwilaya katika Wilaya ya Tarime. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kimsingi tunazo Mahakama za Mwanzo takribani 72 ambazo tuna mpango mkakati wa kuzijenga. Pia, tunazo Mahakama za Wilaya takribani 42 ambazo na zenyewe zipo katika mkakati, ikiwemo na Mahakama ya Tarime. Kwa hiyo, nimhakikishie, kutokana na *characteristics* za Tarime, pale lazima Mahakama iwepo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kadiri fedha itakavyopatikana Tarime ni miongoni mwa vipaumbele vyetu. Kwa hiyo, Tarime ni lazima ipewe Mahakama haraka sana. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza. *(Makofi)*

Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Sasa humu ndani kuna wananchi wanaweza wasielewe hayo makofi yanamhusu nani? Yanamhusu Mbunge ambaye hajaonekana muda mrefu na amekuja leo. Kwa hiyo, tunafurahi kwamba ameungana nasi. Mheshimiwa Asha Mshua, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nakushukuru sana wewe na Bunge zima kwa jinsi

mlivyonichukulia na mlivyonipenda na mlivyonihifadhi mpaka leo Mshua nimeingia ndani ya Bunge lako. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, majengo ya Mahakama yapo ya kutosha tunashukuru, lakini kuna wananchi wengi bado wanapata shida na usumbufu kufuatilia kesi zao ambazo zinapigwa danadana kwa muda mrefu. Je, ni lini Serikali itatengeneza *hotline* au kitengo maalum kwa watu wanaopata shida, wanaofuatilia kesi zao *indefinitely* kesi ndogo ndogo kama za upangaji, mtu kapanga nyumba halafu hataki kuhama, wala hataki kulipa? Lini Serikali itawasaidia wananchi hawa kuondoa kero yao hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, wanasema *a.k.a* Mshua. Suala la kuwa na *hotline* kama alivyosema ni jambo la muhimu, na tayari Mahakama ina *hotline*. Wale ambao wanadhani kesi zao zimecheleweshwa, wanaweza kupiga simu na kuweza kujua taarifa zao.

Mheshimiwa Spika, wakati unatembelea Mahakama walikuonesha hiyo namba ambayo wananchi wanaweza kupiga kuulizia kuhusu kesi. Kwa hiyo, tayari kama anavyosema, *hotline* tunayo. Pia Mahakama hivi sasa tumepunguza *backlog* hadi kufikia asilimia nne. Tunaendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais, ameteua Majaji. Hivi sasa Majaji wameongezeka na Mahakama zetu zimejitahidi kutekeleza kesi kwa haraka sana kwa sababu hivi sasa tunatumia teknolojia *(e-Case Management)* ili kuhakikisha kesi haziendi muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la Mheshimiwa ni la msingi na hivi sasa tuna-*fast track* kesi zisichukue muda mrefu. Tukichukulia Mahakama za Mwanzo huwa hazizidi miezi sita. Ndani ya miezi sita Mahakama za Mwanzo nyingi wanakuwa wameshamaliza shauri, inabaki zile ambazo zinaenda kwa *appeal,* Mahakama za Wilaya au Mahakama Kuu na Mahakama za Rufaa. Kwa hiyo, mkakati wa kupunguza *backlog* unaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, kwani swali Na. 9 la Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ambalo lilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya litaulizwa wakati mwingine. Naipa Serikali nafasi ya kuleta upya majibu yao. Kwa hiyo, hili litajibiwa upya katika Bunge letu hili Mheshimiwa Mbunge.

Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 10

**Ujenzi wa Bandari Kavu Tunduma**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Bandari Kavu utaanza katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* inaendelea na taratibu za utwaaji ardhi katika eneo lililotengwa na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduma la takribani ekari 1,600 kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu. Aidha, taratibu za utwaaji ardhi zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na pindi zitakapokamilika, taratibu za ulipaji fidia unatarajia kufanyika katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, ujenzi wa bandari kavu utaanza baada ya kufanya usanifu wa miundombinu ya bandari pamoja na taratibu za ununuzi wa mkandarasi atakayetekeleza ujenzi huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MH. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza; kwa kuwa nchi iko katika ushindani wa kibiashara baina ya mataifa mengine, je, Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha mchakato?

Mheshimiwa Spika, swali langu namba mbili, kutokana na changamoto kubwa ya msongamano wa malori ndani ya mpaka wa Mji wa Tunduma ambayo yanavuka mpaka nataka kujua hatua zilizofikiwa mpaka sasa katika kujenga kituo cha maegesho cha muda ili kuepusha changamoto ya mlundikano wa magari makubwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella Fiyao, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza kuhusu kuharakisha mchakato, Serikali inaendelea kufanya kazi hiyo ya kuharakisha kama nilivyosema, bila kuathiri taratibu ambazo zimewekwa ikiwa ni pamoja na kufanya huo uthamini na baadaye kulipa fidia katika mwaka wa fedha ambao unafuatia.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kuondoa msongamano, hii imekuwa ni changamoto kubwa na ndiyo maana Serikali imefanya mambo mawili makubwa kwa sasa kama unavyofahamu. La kwanza, tayari tumeshakaa kama nchi mbili, Zambia na Tanzania. Hii ilikuwa ni maamuzi yaliyofikiwa na

viongozi wakuu wa nchi kupitia ziara ya Rais wetu alipokwenda Zambia ili tuondoe vikwazo vyote vilivyopo mpakani.

Mheshimiwa Spika, tunaamini suluhu hii ni ya kudumu zaidi pengine kuliko kuweka kipande pembeni pale Tunduma. Pia, Serikali inaendelea na mchakato mkubwa wa kuboresha reli yetu hii yote ili mzigo mkubwa zaidi uweze kubebwa kupitia Reli ya *TAZARA* kutoka Tanzania mpaka Kapiri Mposhi, Zambia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Tabora, Wilaya ya Manispaa, Kata ya Ifucha waliahidiwa kujengewa bandari kavu kwenye mkutano wa hadhara alipokuja Mheshimiwa Waziri Mbarawa; na mpaka sasa hivi Halmashauri ya Manispaa ya Tabora imeshalipa fidia ya heka 600 katika Kata ya Ifucha, je, Serikali inatupa *status* gani wananchi wa Mkoa wa Tabora ili kusubiri kwa hamu ujengaji wa bandari kavu katika mkoa wetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge, dada yangu Munde kwa kuweza kukumbushia jambo hili. Nimhakikishie kwamba Mheshimiwa Waziri ameshanituma katika Bunge hili niende Tabora kwa ajili ya kuona sehemu hiyo ili kuendelea kupanga namna bora ya kufanya kuendana na jambo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Naona una swali lingine. Mheshimiwa Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mbunge wa Ilemela, sasa aulize swali lake.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali la Mheshimiwa Angeline Mabula kwa niaba yake.

**SPIKA:** Mheshimiwa subiri. Ili uweze kuzungumza, ni lazima utambuliwe kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Stansalaus Shing'oma Mabula atauliza kwa niaba ya Mheshimiwa Angeline Mabula.

Na. 11

**Mgogoro wa ardhi kati ya wananchi na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA K.n.y. MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA** aliuliza:-

Je, lini mgogoro kati ya wananchi wa Kiwanja cha Ndege Mwanza na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege - Mwanza utatatuliwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula, Mbunge wa Ilemela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali Kuu kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa ina nia ya dhati na imeendelea na jitihada mbalimbali katika kushughulikia mgogoro huu ili kuhakikisha unaisha. Aidha, taratibu za utwaaji ardhi zinaendelea kwa kufanya uthamini wa mali za wananchi. Pindi uthamini utakapokamilika, taratibu nyingine zitaendelea kulingana na Sheria ya Ardhi pamoja na Sheria ya Uthamini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ilishakuwa na makubaliano ya awali kuchukua eneo ambalo siyo zaidi ya ndani ya mita 700 kulipa fidia na sasa

inaonekana itakwenda zaidi ya kata tano zikiwemo Kata za Shibula pamoja na Bulyanhulu na wakazi zaidi ya 1,400, je, Serikali haioni kuchukua eneo lote hili kwa wakati mmoja kutaathiri maisha ya baadhi ya wananchi ambao wako nje kabisa ya eneo la uwanja wa ndege?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali kwa kuanza ujenzi wa jengo la abiria, ni lini mkakati wa Serikali kuhakikisha Uwanja wa Ndege wa Mwanza na wenyewe unakuwa moja ya viwanja vya Kimataifa hapa nchini? Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la pili kisha nirudi swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inatambua umuhimu wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza kuufanya wa Kimataifa na tayari mambo kadhaa yameanza kufanyika. La kwanza, tuko kwenye hatua za ndani za *documentation*. Ili uwanja uweze kuwa wa Kimataifa, kuna taratibu za kisheria ambazo lazima zizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni pamoja na kuondoa wavamizi wapatao 1,000 katika uwanja huu ili waweze kupisha kiwanja hicho kiweze kuwa salama. Pale kuna milima na maeneo mbalimbali ambayo wananchi wamevamia. Kwa hiyo, huwezi kukifanya cha kimataifa wakati huo huo usalama wa kiwanja uko mashakani.

Mheshimiwa Spika, la tatu, tunafanya kazi ya uboreshaji wa miundombinu. Kama unavyofahamu, tarehe 28 mwezi huu Waziri wetu Mheshimiwa Mbarawa alikwenda kushuhudia ujenzi wa jengo la abiria. Iko mikakati mingi, lakini nimetaja mitatu ya kuufanya uwanja huu kuwa wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, sasa nikirudi kwenye swali lake la kwanza, nafikiri litakuwa limeshajibiwa na hoja hii ya pili, kwa sababu

hatuwezi kuacha eneo ambalo nimeshalisema pale juu, kwa sababu tu tunataka tuufanye uwanja wa kiamataifa. Kwa hiyo, lazima watu wapishe ili tuweze kuupa hadhi inayostahili, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Amina Ali Mzee.

Na. 12

**Kutekeleza Sera ya Matibabu Bure kwa Wazee**

**MHE. AMINA ALI MZEE K.n.y. MHE. TAUHIDA C. GALLOS** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha Sera ya Wazee kupata matibabu bure inatekelezwa katika kila Kituo cha Afya nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wazee wasio na uwezo wa kugharamia huduma za afya wameendelea kupatiwa huduma hizo kwa utaratibu wa msamaha. Hata hivyo, ni kweli kuna changamoto kwenye baadhi ya maeneo. Kuanza kwa utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote itakuwa suluhu ya kudumu katika kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Ali Mzee, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA A. MZEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Je, ni lini Serikali itaanza huduma ya utoaji huduma ya afya kwa wazee?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli utoaji wa huduma za afya kwa wazee unaendelea. Ni kwamba tu tuhamasishane sisi Wabunge, tunapokuwa kwenye majimbo yetu kupitia Serikali ya Wilaya husika na Baraza letu la Madiwani, tushirikiane sote kwa pamoja kusimamia taratibu na kanuni za Serikali ili kila jambo ambalo limeelekezwa kwenye *policy* za Serikali liweze kutekelezwa ipasavyo na watendaji wetu kule chini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 13

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi Bukumbi - Meatu**

**MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi Bukumbi – Meatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Bukundi ina Kituo cha Polisi ambacho kiko kwenye jengo lililoazimwa kutoka Idara ya Mifugo, Halmashauri ya Wilaya ya Meatu. Ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya ya Meatu imetoa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 1,011.5 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Kata. Ujenzi wa kituo hicho utazingatiwa katika mpango wa ujenzi wa Vituo vya Polisi Kata uliondaliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI vitakavyoanza kujengwa nchi nzima kuanzia mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza ya ujenzi wa Vituo hivi vya Polisi na Bukundi itakuwemo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Simon Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza; Kata ya Bukundi ina changamoto kubwa sana, wafugaji wanagombana sana kwa ajili ya maeneo ya kufuga. Kwa hiyo, kule hatuna kituo cha polisi; je, ni lini sasa Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Kata ya Bukundi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Minza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi ni kwamba baada ya bajeti hii ambayo tunayoenda kuijadili kwenye kipindi kinachokuja, awamu ya kwanza itaweka umuhimu wa kujenga Kituo cha Polisi katika Kijiji cha Bukundi. Namuomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo, baada ya bajeti hii tunakwenda kuanzisha ujenzi kwenye eneo lake hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Jeremia Mrimi Amsabi, Mbunge wa Serengeti, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere.

Na. 14

**Ujenzi wa Barabara ya Sanzate – Natta – Serengeti**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE K.n.y. MHE. JEREMIAH M. AMSABI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya lami kipande cha Sanzate hadi Natta.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa Barabara ya Sanzate – Natta, urefu wa kilometa wa kilometa 40 ambapo hadi kufikia Machi, 2024 utekelezaji umefikia asilimia 45 na mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Januari, 2025, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu ya Serikali, hii Barabara ya Sanzate - Natta inanihusu na mimi Mbunge wa Bunda. Kwa kuwa, Waziri amekuja mara mbili au mara tatu kwenye barabara hiyo na hakuna majibu yanayoendelea; na kwa kuwa, mkandarasi analalamika ameleta *certificates* tisa hazijalipwa mpaka sasa.

Je, ni lini Serikali itamlipa mkandarasi huyu *certificate* hizi aweze kumalizia barabara hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna kipande cha kutoka Natta kwenda Mugumu, je, Serikali ina mkakati gani wa kumalizia kipande hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya Mheshimiwa Waziri kutembelea na kuongea na mkandarasi pia kimefanyika kikao cha Mkandarasi na Watendaji wake Wakuu ambapo tunavyoongea sasa hivi kumekuwa na mabadiliko na mkandarasi ameshakuwa yuko *site*, anajenga na sasa anaanza kuandaa daraja na kuandaa *material* kwa ajili ya kukamilisha barabara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari maandalizi ya malipo ya *certificate* za mkandarasi huyu yapo na ndiyo maana amesharejea *site*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Barabara ya Natta – Mugumu, tutakuwa tunakamilisha kipande hiki, tumeendelea kujenga kwa awamu, lakini mpango wa Serikali ni kuijenga barabara yote ili kutoka Mugumu - Natta- Sanzate hadi Makutano barabara yote iwe ya lami. Kwa hiyo, mpango wa Serikali upo kukamilisha hicho kipande, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaona wote mliosimama hapo, lakini muda wetu umekwenda sana. Mheshimiwa Anton Mwantona swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kutoka KK – Iponjola – Ikuti - Kafwafwa hadi Ibungu kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ni barabara ambayo ipo kwenye Ilani kuhakikisha kwamba katika kipindi hiki tunafanya usanifu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunavyoongea sasa hivi, kutoka Kimwa hadi Kafwafwa Mkandarasi Mshauri yuko *site* kwa ajili ya usanifu na upande wa Kafwafwa hadi Ibungu tayari wako kwenye hatua za manunuzi kwa ajili ya kufanya usanifu ikiwa ni maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga upya barabara ya kutoka Tingi kwenda Kipatimu iliyoharibiwa vibaya sana na mafuriko yaliyotokea juzi ili iweze kupitika kama ilivyokuwa zamani?

**SPIKA:** Umeshaeleweka Mheshimiwa, umetaja barabara umeshaeleweka swali lako. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ya Tingi hadi Kipatimu, barabara ni nyingi sana ambazo zimeathirika na mafuriko. Tunafanya tathmini ya barabara zote ambazo zimeharibika na tayari tumeshaanza kuzikarabati ili zipitike, lakini tukiwa tumeshaomba fedha kurejesha hali ya barabara ilivyokuwa awali baada ya msimu wa mvua, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, ni lini barabara ya lami kutoka Kilindoni mpaka Rasi Mkundi Wilayani Mafia, Mkoani Pwani itakamilika kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, katika Kisiwa cha Mafia ndiyo barabara pekee kuu. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba iko kwenye mpango kwa mwaka huu kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, kutokana na mvua nyingi zinazonyesha, madaraja 12 yamesombwa na mafuriko katika Bonde la Ziwa Rukwa; je, ni lini Serikali itaenda kurekebisha madaraja yale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Binafsi nimeshatembelea eneo hilo, ni kweli limeathirika sana na lina madaraja mengi. Tunachofanya sasa hivi ni kurejesha mawasiliano kwa muda kwa sababu barabara inaendelea. Meneja wa Mkoa tayari yuko *site* anafanya tathmini ya ukubwa wa gharama ya madaraja hayo kuyarejesha ili tuweze kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshaomba fedha kwa Mheshimiwa Rais zaidi ya shilingi bilioni 200 mpaka Februari ambazo zitasaidia kurejesha mawasiliano ya barabara zote. Nadhani Mheshimiwa Rais ameshatoa hela shilingi bilioni 66 kwa ajili ya *emergency* ili kurejesha mawasiliano. Tunategemea baada ya hapo barabara zote zitahitaji shilingi bilioni 200 hadi Februari. Kwa kuwa bado mvua zinaendelea kunyesha, kwa hiyo tutaendelea kufanya tathmini, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba barabara ya Nachingwea – Masasi - Liwale alisema ujenzi wake utaanza kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha. Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri alisema wanatafuta mkandarasi wakati tayari mwaka jana mwezi Juni tulisaini

mkataba kwa ajili ya mkandarasi. Nataka kusikia kauli ya Serikali, mkandarasi amepatikana au bado hajapatikana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale, kilometa 175 mkandarasi amepatikana, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini Barabara ya Karatu – Kilimapunda – Mbulu ujenzi wake utaanza kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge itajengwa kama tulivyopanga kwenye kitabu chetu cha bajeti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itakamilisha kipande cha Amanimakoro – Ruanda ambacho muda wake umekwisha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba mkandarasi yuko *site* na Waziri ametembelea. Tumeongea na mkandarasi huyo kuondoa changamoto ambazo zilikuwa zinamfanya achelewe. Kwa hiyo, tuna uhakika baada ya majadiliano tutamwongeza muda ili aweze kuijenga hiyo barabara yote kwa kiwango cha lami kwa sababu tayari yuko *site,* ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ni lini Mheshimiwa Waziri atatembelea Wilaya ya Kilwa kujionea barabara za *TANROADS* ambazo zimeharibika na mvua na hatimaye kuzipatia ufumbuzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu kutembelea barabara zote. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kama tutapata nafasi muda wowote twende tukazitembelee hizo barabara, aidha mimi au Mheshimiwa Waziri mwenyewe, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara ya Haydom – Mbulu tumesaini mkataba mwaka jana mpaka leo haijajengwa. Je, lini wanawapa pesa wakandarasi ili wajenge barabara ile?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshasaini barabara na mkandarasi tayari amesha-*raise certificate,* lakini alikuwa na changamoto yeye mwenyewe katika kampuni yake ya kiuongozi ambayo tayari ameshaitatua. Tuna hakika baada ya kipindi hiki cha mvua kasi itaanza kwa ajili ya kujenga hiyo barabara, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itakwamua ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ya kipande cha *Kibondo Town Link* ambao umesimama kwa zaidi ya miezi mitano sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimetembelea hiyo barabara kilometa 25 kulikuwa na changamoto ya malipo. Tayari wenzetu wa Wizara ya Fedha wanaandaa malipo ili mkandarasi aweze kukamilisha kipande hicho cha *Kibondo Town Link* chenye urefu wa kilometa 25, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo Ramadhani, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ni lini sasa Serikali itaanza rasmi ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya kutoka Singida Mjini - Hydrogas - Ilongero ambayo tuliahidiwa hapa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Singida – Ilongero nadhani kilometa 10 au 12 zimeshapata kibali cha kutangazwa. Kwa hiyo, muda wowote zitatangazwa ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, sasa aulize swali lake.

Na. 15

**Kuondolewa biashara ya maduka ya kubadilisha fedha nchini**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Je, sababu gani zilisababisha maduka ya kubadilisha fedha kuondolewa katika biashara na wananchi wengi kupoteza ajira zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016, Benki Kuu ya Tanzania ilifanya ukaguzi wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni na kugundua miamala mbalimbali kwa baadhi ya maduka kinyume na matakwa ya sheria na kanuni za usimamizi wa maduka ya fedha za kigeni na udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu. Kufuatia hali hiyo, mwaka 2018 na 2019, Benki Kuu kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali ilifanya *operation* ya ukaguzi maalum kwenye maduka yote ya kubadilisha fedha za kigeni nchini na kubaini makosa mbalimbali ikiwemo:-

(i) Kutofanya utambuzi wa wateja kabla ya kutoa huduma kinyume na kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji Fedha Haramu, Sura 423 na kanuni ya 17 ya Kanuni za Udhibiti wa Utakatishaji Fedha Haramu;

(ii) Kugawa miamala ya wateja kwa lengo la kukwepa kutunza kumbukumbu muhimu zinazoonyesha uhalali wa miamala kinyume na Kanuni ya 23(4) ya Kanuni za Biashara ya Kubadilisha Fedha za Kigeni, 2015;

(iii) Kutokutoa stakabadhi za miamala kinyume na Kanuni ya 23(1) ya Kanuni za Biashara ya Kubadilisha Fedha za Kigeni, 2015;

(iv) Kutokuwasilisha taarifa sahihi za miamala Benki Kuu na hivyo kuathiri upatikanaji wa takwimu muhimu kwa ajili ya shughuli za kiuchumi; na

(v) Baadhi ya maduka yalikuwa yanajihusisha na uhamishaji wa fedha nje ya nchi bila kuwa na kibali au leseni kutoka Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya operesheni hiyo, Benki Kuu ya Tanzania ilibatilisha leseni za maduka ya kubadilisha fedha za kigeni yaliyokutwa na makosa. Maamuzi hayo yalifanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 36(1)(b) na 2(d) ya Kanuni za Biashara ya Kubadilisha Fedha za Kigeni, 2015 iliyorejewa mwaka 2019, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Pondeza, nimekutazama naona umeketi, umeridhika na majibu siyo?

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, hapana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa vile majibu mazuri ya Serikali Naibu Waziri amesema kama kuna maduka yalikuwa yamefungwa na Serikali kutokana na utakatishaji wa fedha. Yako maduka ambayo yamefungwa na baadaye ikajulikana kama hayana makosa hayo ya utakatishaji wa fedha. Je, Serikali iko tayari kuwarudishia wale ambao walifungiwa lakini hawana shutuma hizo za utakatishaji wa fedha ambao fedha zao na mali zao zilizochukuliwa na Serikali?

Mheshimiwa Spika, la pili, je, ni lini sasa wale wote ambao wameonekana hawana hatia maduka yao yatafunguliwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan haiko tayari kuona kwamba kuna rasilimali fedha ya mtu au rasilimali yoyote imebaki Serikalini kumnyima mtu huyo haki yake. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wale wote ambao wameonekana maduka yao hayana makosa yoyote watarejeshewa fedha zao na rasilimali nyingine zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, maduka yaliyosalia, maduka yote ambayo yamefungwa yalikuwa ni 68 wakati ule. Maduka yaliyobaki sasa ni maduka saba tu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika hayo saba yatafunguliwa muda wowote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Naungana naye kuongeza taarifa kwamba hiki alichokisema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Serikali ya Awamu ya Sita haiko radhi kuona fedha za raia mwema zinashikiliwa na Serikali. Kwa kipande kingine kulikuwa na *component* ya kodi ambayo ilikuwa imezidishwa, niongezee na hiyo kwamba kile kipengele cha kodi ambayo ilikuwa imezidishwa tayari kilisharejeshwa kwa wale waliokuwa wanahusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki alichosema Mheshimiwa Naibu Waziri na chenyewe kitaendelea kwa wale ambao walikuwa na baadhi ya vitu ambavyo vilikuwa kwenye mikono ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha hizi Serikali imekaa nazo kwa muda mrefu na kwa kuwa fedha hizi zilikuwa ni za biashara. Je, wakati inarejesha fedha hizo zitaambatana pamoja na riba? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnesta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali haitorejesha fedha hizo kwa riba kwa sababu wafanyabiashara walifanya makosa na wenyewe wamekiri makosa hayo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, kuna ambao hawakufanya.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo nasema Serikali italiangalia suala hilo.

**SPIKA:** Waheshimiwa mkiendelea sasa nyongeza juu ya nyongeza halafu kabla hamjaruhusiwa na mimi sasa hapo…

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali, yapo mambo machache hapa halafu nitaleta matangazo.

Kwanza ni mambo mawili yanayohusu maswali, nimeagiza swali namba sita ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila kwamba Serikali ilete majibu tena, lakini nimeletewa hapa ufafanuzi ambao nafikiri Mheshimiwa Mbunge anapaswa kupewa ili swali lake liweze kujibiwa vizuri.

Swali lilikuwa linauliza; je, Serikali imefanya utafiti kubaini sababu zilizopelekea wakulima kupata hasara katika mavuno ya mwaka 2022/2023. Sasa kwa sababu mavuno yanakuwa ni ya mazao mengi na kama Serikali inapaswa kuleta jibu la namna hii basi haitaleta jibu kwa mujibu wa tunavyowapa haya masharti ya kwamba majibu yawe na maneno kadhaa na yasizidi ukurasa huu mmoja na huu ukurasa hautakiwi kujaa, hawawezi kutosheleza hayo majibu. Wao wakaamua kuchagua kwa

sababu swali ni la jumla, wakachagua eneo la chakula pekee, wakaleta haya majibu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ili Mheshimiwa Mbunge aweze kujibiwa kile alichokusudia yeye kuuliza, Mheshimiwa Mbunge kwenye hili swali lako hasara katika mavuno mwaka huu sawa, lakini ya zao gani au mazao gani ili Serikali ijielekeze maalum kwenye hilo eneo, kwa sababu likiwa swali la jumla na wao wanachagua eneo mojawapo ambalo wanaweza kuliletea majibu, kwa hiyo, nadhani kwa ufafanuzi huu, utalileta hilo swali lako, litapokelewa na litafanyiwa kazi.

Waheshimiwa Wabunge, swali lingine ambalo limeahirishwa kujibiwa leo ni swali namba tisa ambalo tukishaletewa majibu basi litakuwa sehemu ya maswali ambayo yataulizwa, hilo lilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine linalohusu maswali, kwa sababu muda wetu wa kipindi hiki cha bajeti huwa ni mfupi kwa maswali, nawasihi Mheshimiwa Mbunge ukiwa na swali la msingi, basi maswali ya nyongeza siku hiyo waachie Waheshimiwa Wabunge wenzako, kwa sababu wewe utaonekana mara nne katika kipindi kimoja wakati kuna mwingine amesimama mara kadhaa na sikuweza kumpa nafasi. Mara nne kwa sababu wewe mwenyewe utakuwa umesimama kwenye swali la msingi, halafu ukasimama tena kwenye maswali yako mawili, kwa hiyo hizo ni tatu tayari halafu kuna na hiyo nyingine tena, sasa wengine wanaweza wasipate nafasi.

Waheshimiwa Wabunge, kipindi hiki ambacho muda wetu ni finyu, nawaomba kama una swali la msingi, basi kwenye maswali ya nyongeza wape nafasi Waheshimiwa Wabunge wenzako.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo hapa mbele, kwanza ni tangazo la wageni walioko Bungeni na tutaanza na wageni 91 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Jiji la Dodoma, karibuni sana Bungeni, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani kutoka Mwanza, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 23 na walimu tisa kutoka Shule ya Msingi Salsasha kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wajasiriamali wanne kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linahusu vikao ambavyo kwa kawaida huwa tunafanya siku kama ya jana kama isingekuwa siku ya mapumziko.

Kwanza ni Kikao cha Kamati ya Uongozi, Wajumbe wote tukutane kwenye Ukumbi wa Spika saa 5.00 asubuhi hii. Pia kitafuatiwa na Kikao cha Waheshimiwa Wabunge wote na mimi, kile kikao ambacho huwa tunafanya, tunazungumza yale mambo yanayohusu Uongozi wa Bunge, tutakutana saa 9.00 alasiri, halafu Kikao cha Waheshimiwa Wabunge wote kwa maana *briefing* itakuwa saa 10.00 jioni. Waheshimiwa Wabunge, tuzingatie muda huo ambao tumepewa hapo.

Waheshimiwa Wabunge, bado nimesimama …

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, hatujaelewa.

**SPIKA:** Yaani amezungumza mwalimu na hamjaelewa, basi kweli hakijaeleweka leo. *(Kicheko/Makofi)*

Sawa saa 5.00 asubuhi ni Kamati ya Uongozi, kwa hivyo Wajumbe wa Kamati ya Uongozi tukutane Ukumbi wa Spika saa 5.00 asubuhi; saa 9.00 alasiri Waheshimiwa Wabunge wote watakutana na Mheshimiwa Spika kujadili yale mambo yanayohusu Bunge na Utawala; na saa 10.00 jioni ni Kikao cha cha Waheshimiwa Wabunge wote ambacho huwa Mwenyekiti ni Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nadhani tumeelewana sasa? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo moja linalostahili kutolewa ufafanuzi kwa sababu lilizungumzwa nanyi Wabunge, lakini pia wananchi nafikiri pengine kuna mahali ambapo taarifa haikuwafikia sawasawa wakawa wanaona kuna changamoto kati ya mashirikiano ya Bunge na Serikali, na hili linahusu kampuni ambayo ilikuwa inasimamia uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro *(KIA)* ambayo ilikuwa inaitwa *Kilimanjaro Airport Development Company (KADCO)*.

Waheshimiwa Wabunge, sitaenda kwa kirefu kwa sababu sote tupo humu Bungeni na tumeshazipitia hizo taarifa na tunafahamu mpaka tukafika kwenye maamuzi hayo, lakini kwa kifupi ni kwamba Novemba, 2022 wakati Bunge likijadili Taarifa za *CAG*, Kamati yetu ilikuwa imeshalipitia hili jambo na ikaleta hapa kama mapendekezo na Bunge likaazimia kwamba ule uwanja badala ya kuendeshwa na *KADCO* badala yake uendeshwe na *TAA* kama viwanja vingine ambavyo vinaendeshwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maazimio hayo ambayo yalitolewa tena mwezi Novemba, 2023 Kamati ikarejea na hilo jambo na upande wa Serikali tukatoa nafasi hapa Bungeni kwa ajili ya ufafanuzi na ufafanuzi uliotoka ni kwamba kulikuwa na mkataba mmoja ambao ulikuwa bado, nadhani mnakumbuka kulikuwa na maswali na majibu pale, mkataba mmoja wa upangaji ulikuwa bado. Baada ya yale maswali na majibu hapa, tukakubaliana kwamba ule mkataba kwa sababu Kampuni ya *KADCO* inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 na viwanja vingine vyote vinaendeshwa na *TAA*, huu uwanja urejee *TAA*.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya muda mfupi Serikali ikalifanyia kazi jambo hili na Wajumbe wa Kamati yetu ya Miundombinu wakiongozwa na Mwenyekiti walienda kushuhudia makabidhiano kati ya *TAA* na *KADCO*, kwa maana ya *KADCO* kukabidhi uendeshaji wa uwanja wa *KIA* kwa *TAA*.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo sasa kwa utaratibu wa kawaida, Bunge limemaliza kazi yake ama linakuwa limemaliza kazi yake, mambo mengine ya kiutendaji yanakuwa ni ya Serikali. Bunge haliwezi sasa kuanza kuingia huko kuanza

kufuatilia tarehe ngapi, nani amefanya nini, amesaini barua gani, hiyo sasa tutakuwa kidogo tunaenda nje ya ule utaratibu ambao tumejiwekea wa mgawanyo wa mamlaka na madaraka kwa mujibu wa Katiba yetu.

Waheshimiwa Wabunge, changamoto kubwa tarehe 10 Machi *KADCO* ilitoa *notice* kwa wananchi wanaozunguka hilo eneo kwamba wahame katika hicho kipindi ambacho walitoa, sasa wananchi kusoma kwamba ni *KADCO* wakati Bunge lilikuwa limesema hapo ni *TAA,* lakini pia Serikali ilishakabidhi *TAA*, wananchi wangetaraji barua iandikwe na *TAA* na siyo *KADCO*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa muktadha huo ikatokea hiyo labda kwa kufupisha wingi wa maneno, ikatokea hiyo changamoto kwa maana ya kwamba watu wanaona sasa mbona *KADCO* ndiyo inatoa tena maelezo wakati ilishakabidhi, lakini uendeshaji wa ndani ya Serikali na namna wanajipanga kwamba makabidhiano yale sasa sijui niite ya kiuhalisia yanaisha lini, sasa hilo ni suala ambalo sisi kama Bunge hatuwezi kuingia huko labda itokee changamoto.

Waheshimiwa Wabunge, kwa muktadha huo, ule mjadala uliokuwa unaashiria kwamba pengine Bunge limedharauliwa kwa *KADCO* kuandika barua, hilo ni mchanganyiko pengine ni kwa upande wa Serikali na sisi hatuingii kwenye utendaji, lakini kwa maana ya maamuzi, Bunge lilishafanya maamuzi na Bunge lilishashuhudia Uwanja wa *KIA* ukihamia *TAA*. Kwa hiyo, hapa ninavyozungumza na ninyi, Bunge linafahamu kwamba lilishafanya maamuzi kuhusu jambo hilo na hakuna namna Serikali itadharau maamuzi hayo ya Bunge. Hakuna namna Serikali itaenda kinyume na maagizo hayo ya Bunge. Kwa hiyo, haya mengine ambayo pengine yalikuwa yanazungumzwa kwa namna ya hizo hatua za kiutendaji na kwamba pengine ni *headed paper,* ama sijui aliyesaini ni huyo huyo aliyekuwepo kipindi cha *KADCO*, sasa hayo ni mambo ambayo Serikali inaendelea na huo utaratibu wake na ninafikiri katika wiki chache zilizopita, tumeona Mheshimiwa Rais ameshachukua hatua. Siyo kwa sababu watu wamepiga kelele, lakini kwa sababu ni ratiba

zao za utendaji kwa maana ya kwamba yule aliyekuwa Mkurugenzi wa *KADCO* sasa ameelekea *AICC*. Hatujaona Mkurugenzi wa *KADCO* akiteuliwa mwingine kuashiria kwamba *KADCO* bado ipo, kwa hiyo, maana yake huo ni ule mchakato unaendelea sasa wa kuhakikisha *TAA* inashika madaraka hapo *KIA*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wananchi wasiwe na wasiwasi juu ya hilo, Bunge lao linafanya kazi yake inayostahili na Serikali inafanya kwa sehemu yake, yale ambayo kikatiba wanapaswa kufanya Bunge likiwa linaishauri, lakini pale ambapo Bunge limefanya maamuzi, basi Serikali inafuata hayo maamuzi, yale ya utendaji si kazi ya Bunge, kukiwa na changamoto ni kazi yetu kuisimamia Serikali. Hata hili kama itatokea kuna changamoto basi tutashughulika nayo wakati huo, lakini kwa sasa Serikali imepewa muda ikalifanyie kazi jambo hilo na tunaamini tutapata taarifa, Kamati yenu ipo kwa ajili ya kazi hiyo, Mwenyekiti wetu wa Kamati na Wajumbe wote jambo hili wanalifuatilia kwa karibu, kama kutakuwa na jambo la ziada basi Waheshimiwa Wabunge tutajulishwa na wakati huo tutaweza kufanya maamuzi mengine kama yatakuwa ni ya lazima, lakini kwa sasa hali iko hivyo kwamba *Kilimanjaro International Airport* uko chini ya *TAA*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, hayo ndiyo matangazo niliyokuwa nayo hapa.

Sasa kwa sababu tuko katika kipindi cha mfungo wa mwezi Ramadhani na wote tunafahamu muda wetu huwa tunaubadili kidogo kutoa nafasi kwa ajili ya wenzetu ili waweze kuwahi kwa ajili ya hiyo ibada ya *Iftar,* basi, kwa muktadha huo namkaribisha Mheshimiwa Waziri ili tuweze kutengua Kanuni zetu na utaratibu huo utaanza baada ya sisi kama tutakuwa tumeafikiana na atakachokisema Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, karibu.

**2 APRILI, 2024**

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa kibali ili niweze kutoa maelezo ya Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge.

Kwa kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 34(2) na (4) Bunge litakutana hadi saa 7.00 mchana na kusitishwa mpaka saa 11.00 jioni ambapo huendelea kukaa mpaka saa 1.45 usiku linapoahirishwa hadi siku nyingine.

Na kwa kuwa, katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge unaoanza leo, waumini wa dini ya Kiislamu wamo kwenye mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambapo katika kipindi hicho hutakiwa kuswali na kufuturu kila siku ifikapo saa 12.30 jioni.

Na kwa kuwa, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza shughuli zake zilizopangwa kikamilifu na kwa wakati huo huo kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge wa dini ya Kiislamu kuswali na kufuturu kwa wakati muafaka, kwa mujibu wa taratibu za dini yao, inabidi Bunge litengue Kanuni ya 34(2) na Kanuni ya 34(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 174(1).

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge wakati huu wa kipindi cha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani:-

(i) Kanuni ya 34(2) ambayo inaelekeza kwamba Bunge litakutana hadi saa 7.00 mchana ambapo Spika atasitisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa 11.00 jioni itenguliwe na badala yake Bunge linapositishwa saa 7.00 mchana liendelee na shughuli zake ifikapo saa 10.00 jioni badala ya saa 11.00 jioni.

(ii) Kanuni ya 34(4) ambayo inaelekeza kwamba Bunge litaendelea kukaa hadi saa 1.45 usiku ambapo Spika atasitisha na kuliahirisha hadi kesho yake itenguliwe na badala yake Bunge liahirishwe ifikapo saa 12.00 jioni.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu utatumika wakati wa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani tu na baada ya mfungo huo kukamilika Bunge litarejea tena katika utaratibu wake wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono ahsanteni sana, kwa utaratibu wetu sasa nitawahoji, Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kuhusu kutengua kanuni zetu kuhusu muda wa kukutana.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote wameafiki, ahsanteni sana, hoja imepita kwa hiyo muda wetu utaenda kwa sura hiyo.

*(Hoja ya Kutengua Kanuni kuhusu muda wa Bunge kukutana iliafikiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo na kwa kuzingatia lile tangazo la mikutano ya leo ambayo nimewaeleza, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 4.56 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 3 Aprili, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*